Lile Shauku Kubwa

Sura ya 2

Somo la Kusikiza: Agano Jipya 2

Shababa: Kujifunza mkazo wa msingi na makusudi ya Injili hizi nne.

Yesu akawaambia, chakula changu ndicho hiki, niyatende mapenzi yake yeye aliyenipeleka, nikamalize kazi yake.

- Yohana 4:34

Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele. Maana Mungu hakutuma Mwana ulimwenguni ili auhukumu ulimwengu, bali ulimwengu uokolewe katika yeye. Amwaminiye yeye hahukumiwi; asiyeamini amekwisha hukumiwa; kwa sababu hakuliamini jina la Mwana pekee wa Mungu.

- Yohana 3:16-18

Biblia inazungumzia shida ya mwanadamu ya msingi kabisa iliyo ya asili na kubwa – kuwa tumejitalaki wenyewe kutoka kwa Mungu na utengano huo lazima uondolewe na turejeane. Agano la Kale linatuambia kuwa talaka hii ni matokeo ya dhambi – dhambi ya Adamu na Hawa, wazazi wetu. Ujumbe wake unaelezea kwa ufupi suluhisho la shida ya kutengana kwetu na Mungu kwa maneno haya. “Yesu yuaja!” Ujumbe wa Agano Jipya hata hivyo, unaelezea suluhisho kwa shida yetu kutokea mtazamo mwingine. “Yesu Alikuja!” Sababu ya kuja kwake ilikuwa kutoa msamaha kwa dhambi zetu na kutupatanisha na Mungu.

Yesu alikuwa ufunuo mkubwa wa ukweli ambao dunia imewahi pewa. Maoni mengine yote na imani zingine zote lazima vipimwe kwa ukweli aliotupa Yesu. Ukweli ni kwamba Agano Jipya linatuambia kuwa Yesu alikuwa (na bado) ni sura kamili ya Mungu. Kutoka kwa mfungamano huo na Mungu, alitupatia ukweli wote tunaoweza kuelewa kuhusu Mungu. Kwa sababu vitabu vya Injili vinaelezea maisha ya Yesu, kazi zake, na mafundisho yake, vinafanyika vitabu muhimu zaidi katika Biblia.

Yesu alikuwa na juhudi muno katika huduma yake ya kupatanisha mwanadamu na Mungu. Alisema kuwa “chakula” chake kilikuwa ni kutenda kazi ambayo Mungu alimtuma atende. Alikuja kwa sababu Mungu alitaka kuwasiliana nasi kwa njia ambayo tungeweza kuelewa. Hii ndiyo maana ni muhimu kujifunza vitabu vya Injili: kuelewa ujumbe wa Mungu na kupokea suluhisho lake kwa shida yetu ya kutengwa naye.

1. Ukweli au uongo? Injili ni kamilifu kabisa, ikiangazia kila kiwango cha maisha ya Yesu.

2. Ukweli au uongo? Mathayo na Luka ndivyo vitabu vya injili vya pekee ambavyo vinatuambia kuhusu kuzaliwa kwa Yesu.

3**.** Ukweli au Uongo? Injili zote nne zinasisitiza kufa na kufufuka kwa Yesu zaidi ya mambo mengine yote.

4**.** Ukweli au Uongo? Yesu, anayeishi ndani ya wale wanaoamini, bado anaweza kuponya leo.

Ikiwa hujaambiwa lingine la kufanya, basi, chagua jibu moja tu kwa kila swali lifuatalo.

5. Mbona juma la mwisho la huduma ya Yesu ni la muhimu?
   a. Ndiyo sehemu ya pekee ya maisha ya Yesu tunayojua kuhusu.
   b. Hakufanya lolote la muhimu hadi juma hilo.
   c. Alijaribu kuipindua serikali ya Roma juma hilo, ndiyo sababu ya kusulubishwa kwake
   d. Alifanyika "Kondoo wa Mungu" akajitoa kuwa dhabihu kamilifu kwa dhambi za dunia Yote

6. Yesu "alijawa na nini kwa undani zaidi"?
   a. Kujulikana vizuri na kuwa mtu wa ushawishi mkubwa
   b. Kusoma kwa wingi ilivyowezekana ili afanyike mtu aliyetiwa nuru
   c. Kuyatenda mapenzi ya Mungu na kumaliza kazi aliyopewa na Baba
   d. Kutumia mamlaka ya kisiasa vizuri

7. Tendo gani kuu la mwisho ambalo Yesu alizungumzia akiwa na Musa na Eliya katika mlima wa kubadilishwa?
   a. Kifo chake msalabani
   b. Miujiza yake ya uponyaji
   c. Kuandaa watu kumi na wawili wawe tu kama Yeye
   d. Kuwalinda wanyonge na wasiojiweza katika jumia

8. Kusudi la msingi la kufa na kufufuka kwa Yesu lilikuwa nini?
   a. Kuonyesha uungu wake
   b. Kutuonyesha kuwa kifo ni kivuli tu
   c. Kupatanisha hiyo talaka kati ya Mungu na wanadamu
   d. Kutufunza kujinyima na kutoa dhabihu kwa ajili ya wenzetu

9. Yesu aliunganishaje mtengano wetu na Mungu?
   a. Ali "tukomboa" au alitununulia njia ya kurudi katika familia ya Mungu
   b. Alimshawishi Mungu kuwa sisi hatukuwa wabaya sana kama alivyodhania
   c. Alitushawishi kuwa Mungu hakuwa mtakatifu hivyo kama tulivyodhania
   d. Alitufunza namna ya kupata kibali cha Mungu kwa kutumia matendo mema

10. Kazi gani zingine mbali na ukombozi alizozifanya Yesu?
   a. Alituonyesha njia ya kuishi
   b. Alitufundisha ukweli
   c. Alifanya miujiza ya uponyaji, ulinzi, na upeanaji
   d. Yote yaliyotajwa hapo juu

11. Dhibitisho kuu la Agano Jipya ni gani?
   a. Ukweli ya kwamba kila aliyemsikia Yesu alimuamini
   b. Kufufuka kwa Yesu
   c. Miujiza ambayo wanafunzi wa Yesu walitenda
   d. Hakuna dhibitisho. Tunapaswa kuwa na imani iliyo kipofu

Je umepokea ukombozi na maisha mapya ambayo Yesu ametoa? Na je, umepatanishwa na Mungu? Kama ni hivyo, maisha yako yamebadilika vipi kwa kumjua Yeye? Kama bado, basi muulize akusamehe dhambi zako na akufanye mwenye haki kwa Mungu na akusaidie kufuata njia zake.

_____

_____

_____

Mshukuru Mungu kwa baraka zake zote – ukombozi, nguvu zake na uwepo wake maishani mwako, na kila kitu kingine ambacho ametoa kwa sababu yako. Muulize akupe fursa za kutimiza mapenzi yake na kufanya kazi yote ambayo amekuitia kufanya, na kwa msaada wake wa kufanya kazi hizo.

KUZAMA ZAIDI

1. Yesu alipatanisha vipi ile talaka kati ya Mungu na mwanadamu? (Tafakari 2 Wakorintho 5:18-21)

_____

_____

_____

2. Ni vipi vitabu vya Kutoka na Mambo ya Walawi vinachangia ukweli kuwa Yesu alikuja kupatanisha talaka hiyo kupitia kifo chake msalabani? _____

_____

_____

_____

3. Kwa nini nusu ya sura za kwanza za Injili ya Yohana inazungumzia miaka ya kwanza 33 ya maisha ya Yesu, na nusu ya pili ya sura zake zinasungumzia juma la mwisho la maisha ya Yesu? Ni nini lililo la muhimu zaidi kuhusu juma hilo la mwisho? _____

_____

_____

_____

4. Ni vipi kuona huku kunatuambia sababu ya kuja kwa Yesu? _____

_____

_____

_____

5. Taarifa ya maono na malengo ya huduma ya Yesu, yalikuwa nini kulingana na Yesu mwenyewe alivyosema? (Tazama Yohana 4:34; 9:4; 17:4; 19:30) _____

_____

_____

_____

6. Je una taarifa ya maono na malengo yako ya huduma kwa sababu Yesu alikuja maishani mwako? Kama ni hivyo, ni yapi? _____

_____

_____

_____

7. Nia ya saba ya uheri inashikamana vipi na 2 Wakorintho 5:18-19? _____

_____

_____